East African Journal of Swahili Studies, Volume 6, Issue 1, 2023
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1255

**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 6, Issue 1, 2023**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Usawiri wa Mabadiliko ya Ujumi Mweusi katika Nyimbo za Muziki wa Dansi wa Tanzania: 1990-2000

*ElihakiYonazi[1*] na Dkt. Julius Edmund Frank, PhD[2]*

[1] Chuo Kikuu cha AMUCTA, S. L. P. 108, Tabora, Tanzania.
[2] Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, S. L. P. 388, Songea, Tanzania.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: mtengaelihaki@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1255**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*28 Juni 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Nyimbo, Mabadiliko, Ujumi, Ujumi Mweusi, Unusura, Muziki Wa Dansi Wa Tanzania.*

**IKISIRI**

Kila jamii ina ujumi wake. Ujumi wa Afrika huitwa ujumi mweusi. Ujumi wa jamii huweza kupaka mabadiliko kulingana na mpito wa wakati na mwingiliano wa jamii nyingine. Mabadiliko ya ujumi wa kijamii husawiriwa kwenye kazi za kifasihi za jamii hiyo. Makala haya yamechunguza usawiri wa mabadiliko ya ujumi mweusi kwenye nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania. Data ya maktabani ndiyo iliyotumika. Jumla ya nyimbo 20 za kuanzia mwaka 1990-2000 zilikusanywa, ambapo zimetumika nyimbo 5 tu, zilizoteuliwa kimakusudi, kwa kuangalia dhima kuu, na ya kipekee inayojitokeza zaidi kwenye wimbo husika. Nyimbo hizo ndizo zilizotumika katika mjadala wa makala haya. Nadharia ya Unegritudi na Uhalisia zimetumika katika uchambuzi wa data ya utafiti. Nadharia ya Unegritudi ilituongoza katika kuchambua vipengele vya ujumi mweusi vinavyojitokeza kwenye nyimbo teule. Naharia ya Uhalisia ilituongoza katika kujadili uhalisia wa jamii ya Watanzania na nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania. Aidha, katika kubainisha mabadiliko ya ujumi mweusi, na jinsi mabadilko hayo yanavyosawiriwa kwenye nyimbo teule. Matokeo ya utafiti yanabainisha kuwepo kwa mabadiliko mengi ya ujumi mweusi yaliyosawiriwa na nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania kwa mawanda mapana. Mabadiliko hayo ni kama vile, kukosekana/kupungua kwa; maadili mema, umoja na ushirika, utu; heshima, na adabu na utii. Kutokana hayo, watunzi wa nyimbo hizi wanashauriwa kutunga nyimbo zinazosawiri ujumi mweusi, na kuepuka athari hasi za utamaduni wa nje, ili nyimbo hizo ziweze kukubalika na jamii yote, na kuwa na manufaa endelevu katika jamii yao.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1255

**APA CITATION**

Yonazi, E. & Frank, J. E. (2023). Usawiri wa Mabadiliko ya Ujumi Mweusi katika Nyimbo za Muziki wa Dansi wa Tanzania: 1990-2000 *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 194-208. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1255.

**CHICAGO CITATION**

Yonazi, Elihaki and Julius Edmund Frank. 2023. "Usawiri wa Mabadiliko ya Ujumi Mweusi katika Nyimbo za Muziki wa Dansi wa Tanzania: 1990-2000". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 194-208. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1255.

**HARVARD CITATION**

Yonazi, E. & Frank, J. E. (2023) "Usawiri wa Mabadiliko ya Ujumi Mweusi katika Nyimbo za Muziki wa Dansi wa Tanzania: 1990-2000", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 194-208. doi: 10.37284/jammk.6.1.1255.

**IEEE CITATION**

E. Yonazi & J. E. Frank, "Usawiri wa Mabadiliko ya Ujumi Mweusi katika Nyimbo za Muziki wa Dansi wa Tanzania: 1990-2000", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 194-208, Jun. 2023.

**MLA CITATION**

Yonazi, Elihaki & Julius Edmund Frank. "Usawiri wa Mabadiliko ya Ujumi Mweusi katika Nyimbo za Muziki wa Dansi wa Tanzania: 1990-2000". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Jun. 2023, pp. 194-208, doi:10.37284/jammk.6.1.1255.

## UTANGULIZI

Nyimbo katika jamii ya mwanadamu zilianza zamani sana. Senkoro (1988) anasema kuwa nyimbo ni mojawapo ya utanzu mkongwe sana, zilianza pale tu mwanadamu alivyopata lugha yake, zikiwa na dhima mbalimbali. Mulokozi (1996), Wamitila (2004), na Samwel, Amina na Akech (2013), wanasema nyimbo ni tungo zenye mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka, huundwa na lugha ya mkato, matumizi ya picha na mapigo ya sauti. King'ei na Kisovi (2005) wanaeleza kuwa kuna aina kuu mbili za nyimbo; nyimbo za asili na zile za kisasa. Nyimbo za asili ni nyimbo za kijamii ambazo zimekuwako tangu kale katika jamii mbalimbali. Nyimbo hizi hazina mmiliki, bali ni mali ya jamii nzima, na mtunzi wake hajulikani. Kwa upande wake, nyimbo za kisasa ni nyimbo zilizoanza Tanzania baada ya ujio wa wakoloni, nyimbo hizi huhusisha bendi ya mtu au vikundi fulani vya watu, ambao huwa ndio wamiliki. Tofauti na nyimbo za asili, mtunzi wa nyimbo za kisasa hujulikana na hujitangaza. Nyimbo za aina hii hurekodiwa, husambazwa, huuzwa kwa faida, na huimbwa mahali popote, pawe na tukio la kijamii au bila kuwepo. Nyimbo za kisasa zipo katika aina mbalimbali kutegemeana na eneo na utamaduni wa jamii. Kwa mfano; *reggae* - Jamaica, *sokous* na sebene –Kongo, na nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania –Tanzania.

Assen (2012), Laswai (2015) na Mahenge (2021) wanaeleza kuwa nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania, ni aina ya nyimbo zinazotokana na nyimbo za muziki wa *Sokuos* wa Kikongo. Laswai (2015) anabainisha sifa za nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania kuwa ni; kutumia lugha ya Kiswahili, upigaji wa ala-muziki unaoanza taratibu kusisitiza ujumbe, na kisha kupigwa kwa mwendo wa haraka. Sifa nyingine ya nyimbo hizi ni kuhusisha kikundi cha watu (bendi), na hupigwa moja kwa moja jukwaani. Muziki huu pia hujulikana kama muziki wa Waswahili, hii ni kwa sababu hutumia lugha ya Kiswahili. Bendi nyingi za muziki huu zilianzia maeneo ya mwambao mfano, Dar es Salaam na Tanga (Tanzania). Aidha, muziki huu ulianza kupitia vikundi vya askari jeshini, ambao walikuwa wanapiga bendi zao katika hafla mbalimbali (Kitime, 2013: Laswai, 2015).

Kazi yoyote ya kisanaa hufungamanishwa na ujumi wa jamii yake. Senyamanza (hmk), anaeleza kwamba ujumi ni tawi la falsafa linaloshughulikia dhana ya uzuri, asili ya uzuri, ubaya, utukufu, ufutuhi, ladha na falsafa ya sanaaa. Mawazo ya mtaalamu huyu yanashabihiana na ya Renatus (2018) anaeleza kuwa, ujumi ni uumbuji au urembo katika sanaa. Ujumi hutumiwa kueleza uchunguzi na suala la uumbuji na uvutiaji katika sanaa kwa kujiuliza, nini kinavutia watu, na kwa nini? Semanyaza (kesht.) anaeleza zaidi kwamba, ujumi wa kisanaa hufungamana na vionjo vya mtu na kaida za jamii.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

Ponera (2014) anaeleza kuwa ujumi una dhima ya kutathmini na kuhakiki, na kuhoji sababu zipi zimeipa kazi fulani ya kisanaa ubora. Aidha, kama kazi ya kisanaa ina kasoro huhakiki sababu zake, na kuelezea umuhimu wa kasoro ya kazi hizo kwa jamii. Ubora au ubaya wa kazi fulani ya kifasihi hupimwa kwa kufuatana na idili za jamii husika na mazingira yake. Ponera (kesht.) anasema, ujumi hujishughulisha na kutathmini uzuri au ubora wa sanaa, kwa upande mwingine udhalili wa sanaa hizo. Hii ni kwa sababu uzuri hauwezi kuwepo kama hakuna ubaya.

Ujumi hutumika kama kipimo cha ubora au uzuri wa kazi za kisanaa kulingana na jamii husika. Kila jamii ulimwenguni ina ujumi wake unaotofautiana na ujumi wa jamii nyingine, kulingana na utamaduni na mazingira yake (Luhwago, 2013). Jamii za Afrika zina ujumi wake mahususi uliokuwapo tangu kale, uliotumika katika kutathmini na kuhakiki fasihi yake. Ujumi huo hufahamika kama ujumi mweusi. Zirimu (1973) anasema ujumi mweusi ni uzuri wote wa kiujumi utokanao na jamii ya Kiafrika pamoja na mazingira yake. Aidha, huhusisha vigezo vitumikavyo kuainisha urembo wa sanaa kutokana na mazingira ya Waafrika. Ujumi huu hutumika kuzichambua kazi za kisanaa za Kiafrika kwa kuzingatia; ustaarabu, mila, utamaduni, na mazingira ya Kiafrika. Renatus (2018) anaeleza kuwa ujumi mweusi ni uzuri wote unaopatikana katika mazingira ya jamii za Kiafrika kutokana na utamaduni wao. Kwa upande wao Mihale (2011) na Sanga (2012) wanafafanua zaidi dhana hii kwa kusema ujumi mweusi ni nadharia au mkabala wa kushughulikia fasihi na sanaa mbalimbali za Kiafrika. Aidha, Wamitila (2003) anaeleza kwamba fasihi ya Afrika ina ujumi wake mahususi unaojidhihirisha katika vipengele vikuu vinne ambavyo ni; wahusika, madhari, matumizi ya lugha, na utendaji. Njogu na Wafula (2007) wanakubaliana na Wamitila (2003), kuhusu uwepo wa ujumi mweusi, kwa kueleza kwamba, ujumi mweusi ni vigezo vinavyotumika kuainisha urembo wa sanaa kutokana na mazingira ya watu weusi.

Sanga (2012 & 2018), Laswai (2015) na Renatus (2018) wanabainisha vipengele vinavyoonesha ujumi mweusi kuwa ni; umoja na ushirika, imani za kidini, utii na adabu, utu, uhalisia, ukizinda, makusudio, ushababi pamoja na lugha. Zirimu (1973) anaeleza zaidi kwamba ujumi mweusi huchanganua; maudhui, mbinu za wahusika (utendaji), mbinu za uandishi pamoja na lugha. Kwa upande wa lugha hujumuisha maeneo kama vile; misemo, methali, na kinaya.

Bukenya, Gachanja na Nandwa (1997) wanaeleza kwamba ujumi huweza kutumika kama mkabala wa uhakiki wa kazi za kifasihi, na kuonesha ubora au udhalili wa kazi hizo. Aidha, Njogu na Wafula (2007) wanaeleza kwamba ujumi mweusi hutumika kuzichambua kazi za sanaa za Afrika kwa kuzingatia; ustaarabu, mila, tamaduni, na mazingira ya Kiafrika. Russel (2012), John (2018) na Sanga (2021) wanasema kuwa ujumi mweusi una dhima kubwa sana kwa jamii za Waafrika. Wanaeleza dhima hizo kuwa ni; kuelezea idili za jamii ya Waafrika na utathmini wa maisha ya kila siku ya Waafrika. Aidha, wanafafanua zaidi kwamba dhima hizi husawiriwa katika kazi za kifasihi za Kiafrika, na kusababisha kazi hizo kuwa kubalifu zaidi. Aidha, Mulokozi (2017) anasema kuwa ujumi katika kazi za kifasihi una dhima za kijamii na zile za kiburudani. Anafafanua kwamba ujumi katika kazi za kifasihi huakisi na kuelezea idili za jamii yake, kwa upande wa pili kuifanya kazi hiyo iwe na uzuri kufuatana na jamii yake, hivyo kugusa hisia za wanajamii.

Mabadiliko ya ujumi kwa mujibu wa Marx, huwa ni suala lisilo la hiari ya mtu au mwanajamii, bali ni hali isababishwayo na uhitaji pamoja na nguvu vimkabilivyo mtu hata akakosa uhuru wa kuamua katika kusana kazi yake. Wafuasi wa mawazo ya Marx katika fasihi wameainisha maeneo makuu matatu ambayo mabadiliko ya kiujumi hutokea; Mkengeuko kati ya mwandishi na asili yake, katika nafsi, na kati ya msanii na kazi yake (Sanga, 2018).
Wamitila (2010) na Mbawala (2011) wanaeleza kwamba, mabadiliko ya kiujumi husababishwa na uigaji, athari, pamoja na mpito wa wakati. Mabadiliko ya kuiga huweza kusababisha mkengeuko wa kiujumi katika jamii iliyoiga (Sanga,

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

2018). Aidha, Damrosch (2003) anahusisha utandawazi na mabadiliko ya ujumi mweusi. Anaeleza kwamba katika mfumo wa kiutandawazi, mataifa yenye nguvu yameyaathiri mataifa ya dunia ya tatu kwa kuiga mfumo wao wa kibepari bila uhiari wao. Hivyo, utamaduni wa Kiafrika unaathiriwa na utamaduni wa kigeni kupitia vipengele kama vile; mavazi, tabia, mienendo na vyakula, na hivyo kupata mabadiliko kadhaa.

Damrosch (kesht) anaeleza zaidi kwamba, Waafrika wana kasumba ya kuona kwamba maarifa na kila kitu cha Magharibi ni bora zaidi kuliko vile vya Afrika. Samwel, Amina na Akech (2013) kwa upande wao wanasema, mabadiliko mbalimbali yanayotokea kwenye jamii husawiriwa kwenye kazi za kifasihi za jamii husika. Wanaeleza zaidi kwamba mabadiliko hayo huleta athari kadhaa kwenye kazi hizo.

Utafiti huu ulinuia kuchunguza usawiri wa mabadiliko ya ujumi mweusi katika nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania za kuanzia mwaka 1990 hadi 2000. Kipindi hiki kimeteuliwa kwa makusudi kutokana na mabadiliko mbalimbali yalitokea wakati huu (kuanzia mwaka 1990), hususan kutokana na utandawazi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba jamii yoyote hupata mabadiliko kulingana na mpito wa wakati, pamoja na mwingiliano na jamii nyingine. Mabadiliko hayo huhusisha ujumi wa jamii inayohusika. Aidha, mabadiliko yoyote ya kijamii yanapotokea husawiriwa kwenye kazi za kifasihi za jamii yake (Samwel, Amina na Akech, 2013). Matokeo ya utafiti wa makala haya yanabainisha kwamba ujumi mweusi umepata mabadiliko kadhaa, kutokana na mpito wa kiwakati na mwingiliano wa kijamii. Mabadiliko hayo yamesawiriwa kwenye nyimbo teule, kwa mawanda mapana, na kwa namna mbalimbali.

Maandiko ya wataalamu hawa yalitupa mwanga juu ya uhusiano uliopo baina ya ujumi na jamii yake. Kwamba ujumi wa kijamii una uhusiano na maisha na idili za jamii husika katika maisha yao ya siku hadi siku. Aidha, kwamba ujumi huo husawiriwa kwenye kazi za kifasihi na kwamba una dhima anwai, na muhimu. Kwa upande mwingine yalitupa mwanga wa uelewa juu ya mabadiliko ya ujumi wa jamii (ujumi mweusi), sababu na athari zake. Kwa upande mwingine kwamba mabadiliko ya ujumi, kama miongoni mwa taasisi za kijamii husawiriwa kwenye kazi za kifasihi.

## NADHARIA YA UTAFITI

Uchambuzi wa data ya makala haya umeongozwa na nadharia ya Unegritudi na Uhalisia. Uteuzi wa nadharia hizi ni kutokana na kuwa na uhusiano wa kutegemena na kukamilishana kwa kuzingatia mada ya utafiti wetu.

### Nadharia ya Unegritudi

Wamitila (2003) anaeleza kuwa Unegritudi ni tapo linalosisitiza umuhimu wa kuutukuza na kuusifu utamaduni wa mtu mweusi pamoja na kuionea fahari fasihi yake. Mtaalamu huyu anaeleza kwamba, waasisi wa tapo la Unegritudi ni wanafunzi wa Kiafrika, waliotoka katika nchi za makoloni ya Wafaransa ya Afrika na nchi za visiwa vya Karibea. Wanafunzi hao walikubaliana kuanzisha vuguvugu la kutetea na kujivunia uzuri wa mtu mweusi na utamaduni wake, ikiwemo sanaa yake. Vuguvugu hili lilianza mwaka 1930-1960 (Kabira, 1987). Aidha, vuguvugu hili lilichochea hisia za watu weusi kutoka Afrika na nje ya Afrika kuthamini utamaduni wao, na hali zao na kupinga ukandamizaji wa aina zote (Berrian & Long, 1967). Waasisi hawa walitumia tapo hili katika kuzihakiki kazi za Kiafrika kwa kuzingatia utamaduni na mazingira ya Kiafrika, na kujitoa kwenye mikatale iliyokuwa imezoeleka ya kuhakiki fasihi ya Kiafrika kwa mikabala ya Kimagharibi.

Misingi mikuu ya tapo hili ni; kupinga ukandamizaji, na mtazamo hasi wa Wazungu dhidi ya mtu mweusi, kuuonea fahari weusi, ujitambuzi na udumishaji wa Mwafrika, na kukwepa athari hasi za ki-Ulaya na ki-Marekani. Vilevile husisitiza matumizi ya lugha za Kiafrika katika uandishi wa fasihi ya Kiafrika. Husisitiza kwamba kazi yoyote ya kisanaa lazima ihakikiwe kwa mikabala inayoendana na utamaduni

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

na mazingira yake, ili kukwepa hukumu iliyo na upendeleo (Wamitila, 2002).

Nadharia hii ilitumika katika uchambuzi wa ujumi mweusi unaojitokeza katika nyimbo teule. Hii ni kwa sababu Unegritudi husisitiza uandishi wa kazi za kifasihi za Kiafrika unaojikita kwenye ujumi huo, ikiwemo utamaduni na lugha za Kiafrika. Aidha, hupinga matumizi ya tamaduni za nje, kama vile lugha za kigeni katika uandishi wa kazi za kifasihi. Hivyo, nadharia hii imetusaidia katika kubainisha vipengele vya ujumi mweusi, vinavyojitokeza kwenye nyimbo teule kulingana na misingi ya yake. Hata hivyo, nadharia hii haiwezi kuchambua na kuonesha uhalisia wa jamii, jinsi unavyosawiriwa kwenye kazi zake za kifsihi. Vilevile haiwezi kuelezea mabadiliko ya kijamii na usawiri wake kwenye fasihi yake. Hivyo, jukumu hilo lilifanywa na nadharia ya Uhalisia.

**Nadharia ya Uhalisia**

Snow (1968) anaeleza kuwa nadharia ya Uhalisia iliasisiwa huko Ufaransa mnamo karne ya 19 kwa ajili ya kupinga matamanio ya Kilimbwende yaliyokuwa ya kinjonzi zaidi yakilinganishwa na taabu zilizokuwa zikiwakabili watu. Uhalisia huashiria uwezo wa kusawiri hali kwa kuzingatia uyakinifu wa maisha katika jamii. Huonesha uwakilishi wa uhalisi wa mambo na hali ya kijamii vinayodhihirika katika kazi za kifasihi, huelezea kwamba fasihi inatakiwa kuelezea mambo kwa kuzingatia uyakinifu wa maisha na uwakati (Moore, 1976; Njogu na Wafula, 2007; Badru, 2015).
Miongoni mwa waanzilishi wa Uhalisia ni Gustave Flaubert (1821-1880), Karl Marx (1919-1883), Gyorgy Lucas (1885-1971) na Maxim Gorky (1868-1936). Miongoni mwa misingi ya nadharia hii ni;

- Fasihi isawiri au kueleza mambo kwa kuzingatia uyakinifu wa maisha kiwakati;
- Fasihi ieleze mambo ya kihistoria yenye uwezo wa kusababisha mabadiliko makubwa na yaliyo chanya ya kijamii (Wafula na Njogu (2007).

Pamoja na uzuri wa nadharia hii, haiwezi kuchambua ujumi mweusi unaojitokeza kwenye kazi za kifasihi (nyimbo teule). Hii ni kwa sababu vipengele vya ujumi mweusi huelezewa kwenye misingi ya Uafrika vinavyofafanuliwa na nadharia ya Unegritudi. Hivyo basi, jukumu hili limefanywa na nadharia tangulizi; nadharia ya Unegritudi.

Hivyo, nadharia ya Uhalisia ilitusaidia kuonesha uhusiano wa vipengele mbalimbali vya ujumi mweusi, vinavyosawiriwa katika nyimbo teule, na uhalisia wake katika maisha halisi ya jamii ya Watanzania. Aidha, kuonesha mabadiliko ya ujumi mweusi na usawiri wake kwenye kazi nyimbo zilizotafitiwa. Kwa upande wake nadharia ya Unegritudi ilituongoza kubainisha ujumi mweusi unaojitokeza kwenye nyimbo teule.

## METHODOLOJIA

Makala haya yametumia data za maktabani, ambapo nyimbo 5 za muziki wa dansi wa Tanzania zilizoimbwa kuanzia mwaka 1990 hadi 2000, kati ya nyimbo 20 zilizokusanya zilitumika. Nyimbo hizi zimekusanywa kutoka kwenye kaseti, *You Tube* na santuri. Usampulishaji usonasibu ulitumika kupata nyimbo 5 zilizotumika katika uchambuzi wa data za makala haya. Nyimbo hizo ziliteulia kimakusudi, kwa kuzingatia dhima kuu ya kipekee inayojitokeza zaidi kwenye wimbo husika. Data zilikusanywa kwa njia ya kutalii na kukusanya, utazamaji makini na udurusu wa matini. Nyimbo zilizotumika ni; *Walimwengu*, *Mgumba*, *Kisa cha Mpemba*, *Acha Tamaa* na *Mtu Pesa*. Ufafanuzi na uchambuzi wa data za utafiti uliongozwa na mkabala wa kitaamuli.

## UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

Uwasilishaji wa matokeo ya uchunguzi wa makala haya umegawanyika katika vipengele mbalimbali vinavyoonesha mabadiliko ya ujumi mweusi, na jinsi yalivyosawiriwa kwenye nyimbo teule. Vipengele vilivyosawiri mabadiliko hayo vimebainika kuwa ni; umoja na ushirika, imani za kidini, maadili, utii na adabu, heshima na umakusudio. Vipengele hivyo vimejadiliwa kwa kutolewa mifano kutoka katika baadhi ya beti za nyimbo teule zinazosawiri eneo husika kwa mawanda mapana.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

**Usawri wa mabadiliko ya Ujumi Mweusi katika Nyimbo za Muziki wa Dansi wa Tanzania Kuanzaia Mwaka 1990 - 2000**

Matokeo ya utafiti wa makala haya yanabainisha kwamba yapo mabadiliko mbalimbali ya ujumi mweusi yaliyosawiriwa katika nyimbo teule za kuanzaia mwaka 1990 na miaka ya 2000. Mabadiliko hayo yamebainika kusababishwa na mwingiliano wa utamaduni wa Kimagharibi, kupitia utandawazi. Mwingiliano huo umesababibisha ujumi mweusi kuathiriwa, na hivyo kuonesha mabadiliko katika vipengele vyake mbalimbali, kama ilivyobainishwa hapa chini;

## *Mabadiliko katika Umoja na Ushirika*

Kabla ya athari za mwingiliano wa wageni, umoja na ushirika ulikuwa miongoni mwa kipengele muhimu cha uzuri wa Kiafrika. Kabla ya athari za mwingiliano wa kigeni, shughuli mbalimbali na mipangilio yake katika jamii za Kiafrika zilifanyika kwa namna ya kuendeleza na kudumisha uzuri huo. Mwanajamii aliyejitenga alionekana sawa na 'mchawi', hivyo hakukubalika katika jamii yake. Hali imebadilika katika kipindi cha kuanzia mika ya 1990 (utandawazi), ambapo kwa kiwango kikubwa ubinafsi umeonekana ni uzuri katika ujumi mweusi. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti wa makala haya imebainika kwamba ujumi mweusi umepata mabadiliko kadhaa katika kipindi cha kuanzaia mwaka 1990 na 2000. Mojawapo ya vipengele vilivyobainika kuonesha mabadiliko hayo ni kipengele cha umoja na ushirika. Nyimbo teule zilizoimbwa kipindi hiki zinasawiri tabia ya ubinafsi, ambapo tabia hii imeonekana ni uzuri katika ujumi mweusi, kinyume na ilivyokuwa hapo awali. Tabia hizi ni mabadiliko ya ujumi mweusi. Nyimbo zilizosawiri mabadiliko haya ni kama vile;

> ***Walimwengu,*** ulioimbwa na bendi ya *Twanga Pepeta*; kama waimbaji wanavyoeleza hapa chini;
>
> *Chako ni chako,*
> *Changu ni chako,*
> *Ewe kaka vipi!*
> *Chako ni chako,*
> *Changu ni chako*
> *Ewe kaka vipi ooooh*
> **Chanzo:** Data ya maktabani: Mtafiti; 2023

Katika dondoo ya wimbo huu waimbaji wanabainsha vipengele mbalimbali ya ujumi mweusi vilivyopata mabadiliko, ukilinganisha na ilivyokuwa kabla ya athari ya kiutandawazi kwenye ujumi wa Kiafrika. Wanaeleza kwamba kuna baadhi ya watu hawapendi kushirikiana na wenzao kwa vile walivyo navyo, lakini wakati huohuo hutaka kupewa vya wenzao. Maneno,"chako ni chako, changu ni chako" katika wimbo huu hudhihirisha hali hiyo. Tabia hii huashiria ubinafsi, na kutopenda ushirikiano. Mwanafalsafa Marx anaeleza kwamba mahusiano ya kitabaka ndiyo chanzo cha mkengeuko wa wanajamii pamoja na utamaduni wao, ikiwemo fasihi (Sanga, 2018) Yonazi (2019), unashadidia hoja hii kwa kusema, katika jamii ya Waasu - jamii inayopatikana Kaskazini Mashariki mwa Tanzania, kila mtu alichukuliwa kama mwanajamii mkamilifu kama alionesha tabia za ushirikiano na umoja kwa wenzake. Hivyo, tabia ya ubinafsi, si sifa wala kipengele cha ujumi mweusi. Hivyo hali hii kujitokeza katika ujumi mweusi kupitia nyimbo teule ni ushahidi wa athari za kimabadiliko ya ujumi mweusi kutokana na nguvu za mwingiliano wa jamii za nje.

Nyimbo nyingine ilizosawiri mabadiliko ya ujumi mweusi katika kipengele hiki ni ***Mgumba,*** ulioimbwa na bendi ya *Double M Sound***.** Katika wimbo huu waimbaji wamesawiri tabia ya ubinafsi ya mume wa mhusika Mgumba, ambapo baada ya Mgumba kuhangaika kwa muda mrefu bila ya kupata mtoto, mumewe alimfukuza, kwa masimango; kwa mateke na kumtupia vyombo vyake nje. Aidha, kipindi Mgumba hajafukuzwa wifi zake hawakumsaidia, kinyume chake walikuwa wanamsimanga kwa maneno mengi kama vile "unakula tu na kujaza choo". Hivyo, inaonesha dhahiri kwamba mumewe pamoja na wifi zake hawakumpa ushirikiano katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo lake. Uzuri katika umoja na ushirika kama miongoni mwa kipengele muhimu cha ujumi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

mweusi, unasisitiza watu kusaidiana na kushirikiana katika hali zote; shida na raha. Tabia hii inayoelezewa na waimbaji hawa ni sehemu ya mabadiliko ya ujumi mweusi. Waimbaji wanabainisha;

*Mie mie, jamani mie matatizo*
*Mie mie matatizo yamenikabili mie*
*mume wangu akaoa mke wa pili*
*Muda si mrefu akaniacha eee*
*Kwa kashifa nyingi na mateke juu,*
*na kunitupia vyombo nje*
*Nakuhurumia sana wewe dada*
*Nakuhurumia sana Mgumba wee*
*Nimewsikia wifi zako wakikusimanga*
*Eti wewe wamtia hasara kaka yao*
*Eti wewe wamtia shoti kaka yao*
*Unakula sembe ya bure na kujaza choo*
*Eti wanasema huna faida kwao*
***Chanzo:*** Data ya maktabani; Mtafiti*;* 2023

Ushirika na umoja kama kipengele cha ujumi mweusi ulisisitiza kwamba, tatizo lilipotokea katika jamii, lilichukuliwa kama ni la wote. Hivyo ufumbuzi wake ulihusisha familia nzima au jamii yote. Sanga (2021) anashadidia hoja hii kwa kusema, katika ujumi wa Kiafrika, mambo magumu yaliyowakabili watu kama vile ugonjwa, yalionekana ya kawaida kwa sababu yalishughulikiwa kwa umoja. Katika dondoo ya wimbo huu, suala la Mgumba kutengwa na mumewe na ndugu wa mumewe katika kutafuta ufumbuzi wa ugumba wake, na hatimaye kufukuzwa ni ubinfasi mkubwa. Kitendo cha Mgumba kuachwa ahangaike peke yake na tatizo lake, na hatimaye kufukuzwa kutokana na tatizo hilo, ni kinyume na ujumi mweusi; haya ni mabadilikoya kiujumi – ujumi mweusi, kutoka kwenye umoja na ushirika kwenda ubinafsi. Ndharia ya Uhalisia inasisitiza kwamba, kazi ya fasihi si tuli, husawiri mabadiliko yanayotokea kwenye jamii yake. Jamii inapopata mabadiliko, fasihi yake nayo husawiri mabadiliko hayo.

## *Kukosekana kwa Maadili Mema*

Maadili ni miongoni mwa vipengele vya utu. Utamaduni wa Kiafrika husisitiza wanajamii kuwa na tabia za kiutu kama vile; kuonesha upendo, ubinadamu, maadili mema, kujali na kuwa na maelewano na wengine. Jamii za Kiafrika zilifikiri na kutenda mambo kulingana na utamaduni na muktadha wa jamii yake. Maadili mema ilikuwa ni jambo muhimu ambalo kila mwanajamii alilazimika kulifuata kikamilifu. Kwa mfano, heshima ya ndoa, na kutokuwa na tamaa. Nadharia ya Unegritudi inaelezea kwamba, mojawapo ya misingi ya kazi za kifasihi za Kiafrika ni kuzingatia utamaduni wa Afrika na mazingira yake. Matokeo ya utafiti wa makala haya yanabainisha kwamba jamii za Kiafrika, zimekengeuka kimaadili kwa namna mbalimbali. Hali hii inadhihirisha mabadiliko ya ujumi mweusi. Kupitia nyimbo teule, kwa mfano wimbo wa ***Kisa cha Mpemba,*** ulioimbwa na bendi ya *African Stars***,** waimbaji wanaelezea kukosekana kwa maadili mema kwa kiasi kikubwa. Waimbaji wanabainisha;

*Tabia hii kwa Mpemba huyo,*
*ilikuwa ya kawaida*
*Ila kwa siku moja mwenye mke,*
*kagundua hila zoteee*
*Kibwagizo: Sindima*
*Mzee wa watu katoa kiasi cha mboga,*
*kulingana na uwezo wake*
*Kashangaa kuona,*
*anakula vitu vya bei ya juu*
*Kuliko gharama alizotoa*
**Chanzo**: Data ya maktabani: Mtafiti; 2023

Katika wimbo huu waimbaji wanamwelezea Mpemba kama mtu aliyekosa maadili mema kwa kuwa na mahusiano ya kimapenzi na mke wa mtu. Kwa upande wa pili mke huyo naye anachorwa kama mtu aliyekosa maadili kwa kuisaliti ndoa yake kwa tamaa ya fedha/vitu. Waimbaji wanamwelezea mwanamke huyo kama mtu anayetumia mwili wake kwa ajili ya kujinufaisha. Kuwa na mahusiano ya kimapenzi na mke wa mtu kwa utamaduni wa Kiafrika ilichukuliwa kama ukosefu wa maadili. Hivyo, katika wimbo huu Mpemba pamoja na mke wa mtu, aliyekuwa na mahusiano ya kimapenzi naye, wamebainishwa kama watu waliokosa maadili mema.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

Mojawapo ya athari ya mwingiliano wa tamaduni za kigeni katika tamaduni za Kiafrika ni mmomonyoko wa maadili. Hoffmian (2002) anaeleza kwamba utandawazi wa kiutamaduni ni miongoni mwa eneo lililo na athari kubwa katika ujumi wa Kiafrika. Kupitia utandawazi jamii za Kiafrika huiga tabia mbalimbali kutoka jamii za kigeni hususan Ulaya na Marekani, zinazokinzana na utamaduni wa Afrika. Tabia hizo zinapoingizwa kwenye ujumi mweusi hubainishwa kama mojawapo ya mabadiliko ya ujumi huo. Katika jamii asilia ya Kiafrika, tabia hizi hazikuwepo. Hivyo usawiri wa hali hii kwenye nyimbo teule, hasa zile za miaka ya 1990 hadi 2000 ni ushahidi wa mabadiliko ya ujumi mweusi katika kipindi hicho.

Vilevile katika wimbo wa ***Mgumba*** kama ulivyoimbwa na wanamuziki wa *Double M Sound*, wanaelezea kukosekana kwa maadili, wanabainisha tabia ya mtu kuwa na mahusiano ya kimapenzi na shemeji, au binadumu yake, kama mojawapo ya kipengele cha mabadilio ya ujumi mweusi. Waimbaji wanaeleza;

> *Zawadi ni zawadi, usichague*
> *Zawadi ni zawadi*
> *Ya dada binamu kinyama cha hamu*
> *Zawadi ni zawadi*
> *Kaka yako hayupo shemeji kula wee*
> **Chanzo:** Data ya maktabani: Mtafiti; 2023

Waimbaji wa wimbo huu wanaelezea maadili mabaya yaliyopo kwenye jamii kwa sasa, kama vile mtu kuwa na mahusiano ya kimapenzi na shemeji yake, au binamu yake. Katika mshororo wa tatu katika dondoo ya wimbo huu, waimbaji wansema “ya dada binamu kinyama cha hamu”. Tafsiri yake ni msisitizo wa mtu kuwa na uhusiano wa kimapenzi na binamu yake, huelezewa kwamba ni ufahari! Aidha, katika mshororo wa mwisho waimbaji wanasema “Kaka yako hayupo shemeji kula wee”. Halikadhalika, tafsiri yake ni usisitizwaji wa mke wa mtu kufanya mapenzi na shemeji yake. Waimbaji kupitia wimbo huu wanabainisha kwamba wapo baadhi ya wanawake waliokosa maadili kwa kuwa na mahusiano ya kimapenzi nje ya ndoa zao, na wakati mwingine hata na shemeji zao. Kwa upande mwingine wapo ndugu wa karibu waliokosa maadili kwa kuwa na mahusiano ya mapenzi baina yao.

Jamii za Kiafrika tangu kale ziliheshimu sana ndoa, kila mwanajamii alikatazwa kuwa na mahusiano ya kimapenzi na mke au mume wa mtu. Aidha, kila jamii ilipiga marufuku mtu kuwa na mahusiano ya kimapenzi au kuoana na ndugu, kwa mfano binamu. Ilichukulia kama kufanya hivyo ni laana na aibu. Aidha, kuwa kama kuna magonjwa ya kurithi yangeweza kuendelezwa na kusambazwa kupitia kuoana kwa ndugu; kuzaa watoto wenye matatizo hayo maradufu. Hivyo, kusawiriwa kwa mambo haya kwenye wimbo huu, kwa njia chanya (si kwa kuikemea tabia hiyo) ni eneo mojawapo linalobainisha mabadiliko ya ujumi mweusi, ambao umejitokeza kwenye nyimbo teule za miaka ya 1990 hadi mika ya 2000. Nadharia ya Uhalisia inaeleza kuwa, fasihi hutakiwa kusawiri uyakinifu wa jamii yake kulingana na wakati.

Kukosekana kwa maadili vilevile kumesawiriwa kupitia nyimbo teule kama mabadiliko ya ujumi mweusi kupitia wimbo wa ***Acha Tamaa*** ulioimbwa na bendi ya *FM Academia***.** Waimbaji wa wimbo huu wanaelezea tamaa mbaya ya pesa kama miongoni mwa mabadiliko ya ujumi mweusi. Tamaa mbaya ni ukosefu wa maadili mema kwa sababu humpelekea mtu kutenda mambo maovu, kama vile; ukahaba na wizi. Waimbaji wanaeleza;

> *Binadamu hukubali afanye mambo,*
> *ambayo hata si halali juu ya pesa,*
> *Yuda alimuuza Bwana Yesu,*
> *Kaini alimuua Abel,*
> *vijana wanaopenda sugar mamies,*
> *ukiwauliza, eti pia wanatafuta,*
> *Acha tamaa mwanangu yoh, ...*
> *Wasichana wanaopenda sugar dadies,*
> *ukiwauliza, eti pia wanatafuta,*
> *Kama hutoshambulia tunapotafuta pesa,*
> *Ama shuleni haujaendaa,*
> *maisha mazuri usitamani,*
> **Chanzo:** Data ya maktabani: Mtafiti; 2023

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Katika wimbo huu waimbaji wanaelezea ukosekanaji mkubwa wa maadili kutokana na tamaa ya fedha. Wanaelezea tabia mbaya za wasichana wenye umri mdogo, kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanaume waliowazidi umri kwa kiwango kikubwa au waume za watu, kwa sababu ya tamaa ya pesa. Kwa upande mwingine vijana wenye umri mdogo kuwa na mahusiano ya kimapenzi na mama watu wazima; waliowazidi umri, vilevile kwamba ni kutokana na tamaa ya pesa. Hali nii ni ukosefu wa maadili mema ya Waafrika. Sanga (2018) anasema utamaduni wa Afrika ulijengeka kwenye misingi ya kutii na kuonesha adabu kwa wenye mamlaka, na wenye umri mkubwa. Anaeleza zaidi kwamba, watoto na vijana waliwajibika kuwa na adabu njema kwa waliowazidi umri. Mwanajamii yoyote aliyekosa adabu alionekana mtu asiyefaa kwenye jamii na wakati mwingine alipewa adhabu. Katika dondoo ya wimbo huu waimbaji wanaeleza kuwa wasichana wadogo wanawapenda *sugar dadies*, kwa sababu ya pesa.

Neno *sugar dadies* lina maana mwanaume mwenye umri mkubwa, na mara nyingi mwenye mke, kuwa na mahusiano ya kimapenzi na msichana mwenye umri mdogo kwa ushawishi cha pesa. Kwa upande mwingine waimbaji wanaelezea juu ya *sugar mammies*, ambao kwa upande wake ni wanawake wenye umri mkubwa, na mara nyingi ambao hawajaolewa au wameachika, kuwa na mahusiano ya kimapenzi na vijana mwenye umri mdogo, kwa ushawishi wa fedha. Katika jamii za Kiafrika, kabla ya athari za mwingiliano na tamaduni za kigeni, hususan kupitia utandawazi, wazazi walitakiwa kuwa mfano wa maadili mema kwa vijana wao. Hivyo, ilikuwa ni vigumu watu wazima kuwa na mahusiano ya kimapenzi na vijana wadogo. Jambo hili kwa sasa linaonekana la kawaida, na mara nyingi hufanyika kwa kutumia ushawishi wa fedha. Kimsingi, suala la tamaa mbaya kwa Waafrika lilikatazwa sana. Kila aliyejaribu tamaa mbaya aliadhibiwa na jamii yake. Nadharia ya Unegritudi inasisitiza kwamba fasihi ya Kiafrika huhitajia kusawiri idili za Kiafrika. Kinyume na hapo husemwa imekengeuka. Hivyo, tabia zilizosawiriwa kupitia nyimbo hizi (za miaka ya 1990-2000) zinadhihirisha mabadiliko ya ujumi mweusi.

### *Kukosekana kwa Heshima*

Heshima ni kipengele kingine muhimu cha utu katika ujumi mweusi, ambacho kilisistizwa na kudumishwa katika jamii za Waafrika. Katika idili za Kiafrika heshima ilitolewa kwa kuzingatia rika na uongozi. Kwa mfano, watoto au vijana waliwajibika kuwaheshimu wazazi wao, au watu waliowazidi umri. Kwa upande mwingine, viongozi waliheshimika kwa watu waliowaongoza. Matokeo ya utafiti wa makala haya yanabainisha kwamba katika kipindi cha kuanzia mwaka 1990 (utandawazi), suala la heshima kama ilivyokuwa kabla ya hapo kwa jamii ya Watanzania limebadilika kwa kiasi kikubwa. Nyimbo teule nyingi za kuanzia mwaka 1990 zinaelezea heshima ya mtu kwamba si kutokana na umri au mamlaka yake tu, bali kutokana na uwezo wake wa kifedha. Fedha imechukuliwa kuwa ndio kigezo kikuu cha mtu kuheshimika kwenye jamii, bila kujalisha umri wake au tabia zake. Kimsingi, heshima apewayo mwenye hela (tajiri) hufungamana na maslahi fulani kwa watoa heshima hiyo. Karl Marx anaeleza kwamba katika ulimwengu wa Kibepari kila kitu hufanywa bidhaa (Wamitila, 2002). Kwa mantiki hii, kwenye kipindi cha kuanzia mwaka 1990 kipengele cha heshima katika ujumi mweusi kimebadilika, kigezo kingine kikubwa cha heshima kwa mtu kimebainika ni kutokana na uwezo wake wa fedha. Hii ni tofauti na katika idili asilia za Kiafrika kwamba suala la pesa au mali halikuwa kigezo cha heshima ya mtu. Hivyo, haya ni mabadiliko katika ujumi mweusi. Waimbaji wa *Bendi ya Twanga Pepeta* kupitia wimbo wao wa ***Mtu Pesa*** wanaelezea hoja hii;

> *Kuna usemi wa mababu zetu wasema,*
> *pesa ni maua*
> *Mwenye pesa huabudiwa,*
> *sababu ya pesa zake*
> *Mwenye pesa ana jeuri*
> *Mwenye pesa ni mfalme*
> *Hakuna asiyejua haya niyasemayo oooh!*
> **Chanzo:** Data ya maktabani: Mtafiti; 2023

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

Kupitia dondoo ya wimbo huu inaelezwa kwamba mtu mwenye pesa huheshimika kwa kiasi kikubwa kwa sababu ya pesa zake. Maneno "Mwenye pesa huabudiwa, mwenye pesa ni mfalme" humaanisha heshima ya hali ya juu, anayopewa mtu kutokana na hela zake. Hali hii inaonesha kwamba sualala heshima limebadilika, tofauti na ilivyokuwa hapo awali. Kwa sasa fedha ni kigezo chenye nguvu cha mtu kupewa heshima (heshima ya pesa) tofauti na ambavyo angestahili. Hivyo, matokeo ya utafiti huu yanabainisha kwamba ujumi mweusi umepata mabadiliko mbalimbali, miongoni mwayo ni katika utoaji wa heshima. Nadharia ya Uhalisia inaeleza kwamba kazi za kifasihi hubadilika kufuatana na mabadiliko ya jamii yake; jamii inavyobadilika fasihi nayo husawiri mabadiliko hayo.

Wimbo mwingine uliosawiri suala la ukosefu wa heshima ni ***Mtaa wa Saba*** ulioimbwa na bendi ya *African Stars*. Katika wimbo huu waimbaji wanaelezea ukosefu wa heshima kwa baadhi ya watu siku hizi. Wanatolea mfano kwa wanandoa; kukosa heshima ya ndoa, kama waimbaji wake wanavyoelezea hapa chini;

*Tabia ya mke huyu ilianza tangu kitambo*
*Mume alivumilia na kula mapochopocho*
*kwa shingo upande*
*Oyoooo! Maskini*
*Ndipo siku hiyo*
*baba kamwaga manyanga chini*
*na kumtafuta Mpemba*
*Mpemba kakimbia*
*Mzee wa watu katoa kiasi cha mboga*
*kulingana na uwezo wake x2*
*Nashangaa x2*
*Kuona anakula vitu vya bei ya juu*
*kuliko gharama alizotoa x2*
*Hila za Mpemba*
*kuvunja unyumba wa watu eeee*
*Imekuwa vibaya kwa yule mke*
*asingeweka kitumbua kwenye mchanga*
*Atakula tena vipi eee. Mbona hasara*
**Chanzo:** Data ya maktabani: Mtafiti; 2023

Katika dondoo ya wimbo huu waimbaji wanamwelezea mke wa mtu ambaye amebainishwa kukosa heshima na ndoa yake. Ameelezewa kuwa na mahusiano ya kimapenzi na Mpemba, ambaye alikuwa baba mwenye duka. Alifanya hivyo kwa kurubuniwa kwa kupewa zawadi mbalimbali kama vile vyakula. Kwa upande mwingine Mpemba naye ameelezewa kama mwanamume aliyekosa heshima dhidi ya ndoa ya mtu. Kitendo cha kuwa na mahusiano na mke wa mtu ni ukosefu wa heshima. Utamaduni wa Waafrika husisitiza watu kuwa na heshima, miongoni mwa maeneo yanayohitajia kuheshimiwa ni ndoa (Yonazi, 2019). Suala la ukosefu wa heshima dhidi ya ndoa limeshamiri kwa sasa, miongoni mwa jamii ya Watanzania. Hivyo, suala hili katika nyimbo hizi limesawiriwa kama mabadiliko ya ujumi mweusi.

### *Kukosekana kwa Utii*

Katika jamii za Waafrika utii ulikuwa ni mojawapo ya uzuri wa kiujumi. Watoto/vijana walitakiwa kuwatii wazazi au wakubwa zao. Viongozi nao walitakiwa kupata utii kwa waliowaongoza. Kwa upande mwingine, kila mwanajamii alitakiwa kuitii miungu yao. Ilipotokea mtu amekosa utii aliadhibiwa kwa mujibu wa taratibu za familia au jamii. Kwa upande wake, kutoitii miungu kulisababisha mabaa mbalimbali kwenye jamii, kama vile ukame. Suluhisho lake lilikuwa kufanya matambiko ya kuiomba msamaha. Kwa hali hii, suala la utii lilisisitizwa sana na kudumishwa. Utii ulichukuliwa kama suala muhimu lililojenga ustawi wa jamii (Mhando na Balisdya, 1976)

Matokeo ya utafiti wa makala haya yanabainisha kwamba ujumi mweusi umepata mabadiliko katika kipengele cha utii miongoni mwa jamii ya Tanzania. Mabadiliko haya yamebainika kupitia nyimbo teule. Katika kipindi hiki imebainika utii umepungu/kukosekana miongoni mwa watu. Aidha, suala la utii miongoni mwa watu, kwa kufuata misingi yake kama ilivyokuwa awali limebadilika. Kwa sasa pesa imekuwa na nafasi kubwa kwa mtu kutiiwa. Mwenye hela kila mtu humtii, kutokana na hela zake. Kupitia wimbo wa ***Mtu Pesa***, waimbaji wanaeleza;

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

*Mwenye pesa si mwenzako ooooh x2*
*Anaweza kutenda zuri au baya lile atakalo*
*Sio yeye ni pesa*
*Ni pesa  eeeh, zinazo mzuzuax2*
*Kuna usemi wa mababu zetu wasema, pesa ni maua*
*Mwenye pesa huabudiwa, sababu ya pesa zake*
*Mwenye pesa ana jeuri*
*Mwenye pesa ni mfalme*
*Hakuna asiyejua haya niyasemayo oooh!*
**Chanzo:** Data ya maktabani: Mtafiti; 2023

Waimbaji wanaeleza kwamba utii kama kipengele muhimu cha utu, na ujumi mweusi kwa ujumla umebadilika. Katika jamii asilia ya Kiafrika, kabla ya mwingiliano wa wageni mtu hakupata utii kwenye jamii yake kutokana na uwezo wake wa kifedha au utajiri wake, bali utu wake. Wamitila (2002) katika kuelezea nadharia ya Unegritudi anasema, nadhari hii inasisitiza fasihi ya Kiafrika kusawiri mazingira na utamaduni wa Mwafrika. Kwa sasa, kwa mujibu ya matokeo ya utafiti huu mtu anaweza kupata utii kutokana na hela zake. Katika dondoo ya wimbo huu waimbaji wanaeleza kwamba; *mwenye pesa huabudiwa, mwenye pesa ni mfalme, mwenye pesa ana jeuri*. Maneno haya huashiria kitiiwa kwa mtu kwa kiwango kikubwa sana, kutokana na hela zake. Mulokozi (1996) anasema, suala la utii kwa Waafrika halikuishia tu watu wenyewe kwa wenyewe, bali pia waliwajibika kuitii miungu yao. Anaeleza zaidi kwamba, kwa mfano, mtu au jamii iliyoshindwa kuitii miungu yao ilikumbwa na majanga ya aina mbalimbali. Ili kuyaondoa ilibidi kufanyika tambiko la kuomba msamaha. Suala la utii lilikuwa la kikanuni, na aliyekengeuka aliadhibiwa au kukubwa na matatizo makubwa. Utii lilikuwa jambo la muhimu baina ya watu kwa kuzingatia rika na mamlaka. Aidha, utii wa miungu nao ulikuwa la jambo la lazima. Nadharia ya Unegritudi inasisitiza kwamba kazi za Kifasihi za Kiafrika hutakiwa kufungamna na utamaduni na mazingira ya jamii za Kiafrika. Hivyo utii kwa kigezo cha ukubwa na uongozi ni idili za Waafrika. Kinyume chake, utii kwa mtu kwa kigezo cha pesa ni mabadiliko ya ujumi mweusi.

### *Mabadiliko ya Imani za Kidini*

Imani za dini ni kipengele muhimu cha uzuri wa ujumi mweusi. Wataalamu mbalimbali waliojihusisha na uchambuzi wa ujumi katika utamaduni wa Kiafrika, ikiwemo sanaa yake wanasema sanaa na utamaduni wa Afrika hufungamanishwa kwa kiasi kikubwa na miungu waiabuduyo. Tangu zamani, hata kabla ya ujio wa wageni Afrika ilikuwa na namna yake ya kuabudu kupitia dini zake za kijadi. Hali hii  ilikuwa ni miongoni mwa uzuri wa ujumi mweusi. Baadaye Afrika ililetewa dini za kigeni; Ukirsto na uislamu, kupitia mwingiliano wa jamii za nje, hasa kupitia ukoloni na utandawazi. Namna ya kuabudu katika dini za kigeni ilikuwa tofauti ukilinganisha na ilivyokuwa katika dini za kijadi. Dini hizi zilichukua pahala pa dini za kijadi kwa kiwango kikubwa. Kwa kadri muda ulivyokuwa unaenda tangu kuingia kwa dini hizi za kigeni, ndivyo kuimarika na kushamiri kwake kulivyokuwa kunaongezeka (Mbiti, 2011a). Mgodela (2021) anaeleza kwamba, kwa kadri dini za kigeni zilivyokuwa zinashamiri miongoni mwa jamii za Waafrika ndivyo jinsi imani za dini za kijadi zilivyokuwa zinafifia. Nadharia ya Unegritudi inaeleza kwamba fasihi ya Kiafrika isawiri utamaduni wa Waafrika na mazingira yake, kinyume chake itakuwa imekengeuka. Kwa upande wake, nadharia ya Uhalisia inaeleza kwamba, fasihi ya jamii huyasawiri mabadiliko ya kiwakati yanayotokea kwenye jamii yake. Suala la usawiri wa dini za kigeni, hasa za Kikristo katika nyimbo teule za kipindi cha miaka ya 1990-2000 (utandawazi) kwa mawanda mapana, ni mojawapo ya mabadiliko ujumi mweusi, kupitia kipengele za imani za kidini. Katika wimbo wa ***Mgumba,*** ulioimbwa na bendi ya  *Double M Sound* waimbaji wanaelezea;

*Jamani eee,*
*au kosa langu Mwenyezi Mungu baba*
*kuniumba mgumba,*
*au kosa langu*
*Mwenyezi Mungu baba,*
*kuninyima mtoto oooo*
*Au kosa langu kuvumilia,*
*tulipokuwa juani*
**Chanzo:** Data ya maktabani: Mtafiti; 2023

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

Katika dondoo hii waimbaji wanamtaja Mwenyezi Mungu kwa kuonesha kwamba ndiye wanayemwabudu, na kwamba yeye ndiye mwenye uweza wote. Dini za kigeni zinaamini kwamba Mungu ni mmoja tu. Na kwamba ndiye mwenye uweza na mamlaka yote wa kila kitu. Hii ni tofauti na dini za kijadi ambapo kulikuwa na miungu mbalimbali na kila mungu alikuwa na dhima yake, kama anavyobainisha Mulokozi (1996). Hivyo, kutoka kwenye utaratibu wa kuabudu miungu mbalimbali, kila mmoja ukiwa na dhima yake, kwenda kumwabudu Mungu mmoja tu; Mungu Mwenyezi, imebainika kwamba ni mabadiliko ua ujumi mweusi, kupitia kipengele cha imani za kidini. Kuanzia miaka ya 1990 ndipo ueneaji na ushamiri wa dini za kigeni ulikuwa mkubwa zaidi. Wimbo mwingine uliosawiri mabadiliko ya ujumi mweusi kupitia kipengele cha imani za kidini ni ***Acha Tamaa,*** ulioimbwa na Bendi ya *FM Academia*, kama waimbaji wake wanavyobainisha;

*Binadamu hukubali afanye mambo,*
*ambayo hata si halali juu ya pesa,*
*Yuda alimuuza Bwana Yesu,*
*Kaini alimuua Abel,*
**Chanzo:** Data ya maktabani: Mtafiti; 2023

Waimbaji wa wimbo huu wanaelezea habari za Yesu Kristo, kama ishara ya dini za kigeni. Kimsingi, habari hizi zililetwa na kuenezwa na wageni kutoka nje kupitia ukoloni na utandawazi. Kabla ya hapo jamii za Watanzania ziliabudu miungu yao ya kijadi, iliyobainishwa kwa majina tofautitofauti. Mulokozi (1996), anasema Waafrika walikuwa na dini zao za asili, na waliabudu miungu yao toka zamani. Hivyo kusawiriwa kwa habari za Yesu (mtume wa Mungu, kwa imani za Wakristo) katika nyimbo teule ni udhihirisho wa mabadiliko ya ujumi mweusi kupitia imani za kidini. Nyimbo teule zote za kuanzia mwaka 1990 zimebainika kusawiri mabadiliko ya imani za kidini za kigeni. Huu ndio msingi wa nadharia ya Uhalisia kwamba jamii ikipata mabadiliko katika nyanja zake mbalimbali, basi mabadiliko hayo husawiriwa kwenye fasihi zake za kifasihi.

### *Umakusudio Hasi*

Fasihi ya Kiafrika inatendwa kwa makusudio fulani ya kijamii, tofauti na fasihi ya Kimagharibi, kwa kuzingatia tapo la pili la uhakiki wa kazi za kifasihi, ambapo kwao fasihi ni kwa ajili ya fasihi (Mulokozi, 2017). Matokeo ya utafiti wa makala haya yanabainisha kwamba nyimbo teule zimesawiri mbadiliko mengi kengeushi dhidi ya idili za Watanzania. Mfano, suala la mtu na shemeji yake kuhamasishwa kuwa na uhusiano wa kimapenzi au ndugu wa karibu kama vile mtu na binamu yake, ni ukengeushi wa ujumi mweusi. Waimbaji katika wimbo ***Mgumba*** wanabainisha hili;

*Zawadi ni zawadi, usichague*
*Zawadi ni zawadi*
*Ya dada binamu kinyama cha hamu*
*Zawadi ni zawadi*
*Kaka yako hayupo shemeji kula wee*
***Chanzo****:* Data ya maktabani: Mtafiti; 2023

Kazi za kifasihi kwa mtazamo wa Kiafrika hutakiwa kukemea mambo yasiyoendana na idili za Waafrika, na kusisitiza yale mema. Katika wimbo huu, waimbaji wanashabikia na kuhamasisha mtu kuwa na mahusiano ya kimapenzi na shemeji au binamu yake. Wanasema*;'kaka yako hayupo shemeji kula wee"* Hapa wanamaanisha kuwa kaka mtu hayupo, hivyo mdogo wake afanye mapenzi na shemeji yake. Katika mshororo wa pili waimbaji vilevile wanahamasisha mtu na binamu yake kuwa na mahusiano ya kimapenzi. Aidha, katika mshororo wa kwanza na wa tatu, waimbaji wanaeleza kuwa "zawadi ni zawadi" hapa tafsiri yake ni kuwa suala la mapenzi halina mipaka, kitu ambacho ni kinyume na maadili ya Watanzania. Kazi za kifasihi za Kiafrika zina dhima kuu mbili; za kijamii na za kiujumi. Mojawapo ya dhima za kijamii ni kusisitiza kuadili mema (Mulokozi, 2017). Inapoonekana kazi ya kifasihi ya Kiafrika inahamasisha upotofu wa kimaadili, basi kazi hiyo husemwa inaakisi mabadiliko ya kiujumi. Katika wimbo huu imebainika kwamba unahamasisha ukiukwaji wa maadili mema ya Watanzania, kama vile adabu kwa mtu na shemeji yake, na mtu na binamu yake kufanya mapenzi.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

Nadharia ya Unegritudi inasisitiza kwamba kazi za kifasihi za Kiafrika hutakiwa kuutetea utamaduni wa mtu mweusi (Mwafrika). Kwa upande wake nadharia ya Uhalisia hufafanua kwamba kazi za kifasihi hutakiwa kusawiri uyakinifu wa jamii yake. Kama kazi ya kifasihi haitautetea utamaduni wa jamii yake, basi huo ni mkengeuko (mabadiliko) ya kiujumi katika jamii husika.

**HITIMISHO**

Matokeo ya makala haya yanaonesha kwamba ujumi mweusi umepata mabadiliko kadhaa, hususan kuanzia mwaka 1990 hadi miaka ya 2000. Mabadiliko haya yamesawiriwa kwenye nyimbo teuele zilizotungwa kipindi hiki. Mabadiliko haya yamebainika hasa kusababishwa na sababu za kiutandawazi; hasa mwingiliano wa jamii za nje, hasa Marekani na Ulaya. Hata hivyo, pamoja na mabadiliko haya nyimbo hizi zimeonekana bado zina tija kwa kiasi kikubwa kwa jamii ya Watanzania. Hivyo, inashauriwa watunzi wa nyimbo hizi na vyombo vinavyosimamia sanaa Tanzania kuendelea kutoa miongozo imara ya jinsi ya kuepuka mabadiliko hasi katika kazi hizi yanayosababishwa na utamaduni wa nje. Hali hii itazifanya nyimbo hizi kuendelea kuwa na mashiko na tija zaidi katika ustawi wa jamii ya Watanzania. Aidha, inapendekezwa zifanyike tafiti zaidi katika nyimbo nyingine za kisasa ili kuona jinsi mabadiliko ya ujumi yalivyosawiriwa na nyimbo hizo na/au kuleta athari katika kazi hizo.

**MAREJELEO**


Assen, N. V. (2012). *Resonation Muziki wa Dansi in Dar es Salaam, Tanzania. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa)*. African Language and Culture: Leiden University/African Study Centre.

Badru, Z. A. (2015). *Taswira na Ubainishaji wa Mabadiliko ya Kiujumi katika Vitendawili vya Kiswahili: Mifano ya Vitendawili vya Kiswahili*. Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu (Haijachapishwa): Chuo Kikuu cha Dodoma, Dododma.

Berrian, A. H. na Long, R. A. (1967). *Negritude: Essay and Studies*. Hampton Virginia: Hampton Institute Press,

Bukenya, A. S., Gachanja, M. na Nandwa, J. (1997) *Oral Literature; A Senior Course*. Nairobi: Longhorn

Damrosch, D. (2003). *What is World Literature?* Princeton: Princeton University Press,

Hoffman, S. (2002). "Clash of Globalizations," Foreign Affairs. *Juz. 81*:104-115.

John, B. N. (2018) Uwi ni Sifa ya Ujumi wa Kiafrika? Mifano kutoka Diwani ya Mnyampala, Mashairi ya Saadan na Kivuli cha Mvumo. *Mkwawa Journal of Education Development, Juz. 2*:20-33.

Kabira, M. W. (1987). *Theory of Literature. Black Aesthetics. Nairobi: College of Adult and Distance Learnin*g, University of Nairobi.

King'ei, K. na Kisovi, C. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau,

Laswai, A. (2015). *Ujumi katika Muziki wa Dansi: Nyimbo Teule za Marijani na Ally Choki. Tasinifu ya Shahada ya Umahiri (Haijachapishwa)*. Chuo Kikuu cha Dodoma, Dododma.

Luhwago J. N. (2013). *Ujumi katika Fasihi Simulizi: Mifano kutoka katika Hadithi za Wahehe. Shahada ya Umahiri (Haijachapishwa)*. Chuo Kikuu cha Dodoma, Dododma.

Mahenge, E.G. (2021) Matumizi ya Mbinu ya Usimulizi katika Kuibua Dhamira ya Ukombozi wa Kisiasa Kusini mwa Afrika: Uchunguzi wa Nyimbo Teule wa Muziki wa Dansi nchini Tanzania 1940-1990. *Mulika , Juz* 4 (2): 78-94

Mbawala, A. M. (2011*). Mabadiliko ya Ujumi wa Kifasihi Kulingana na Wakati: Mfano wa Nyimbo Teule za John Komba Mwaka 1980-2000*. Tasnifu ya Shahada ya Umahiri

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

(Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Mbiti, J. S. (2011a). *African Religion and Philosophy*. Kampala: East African Educational Publisher Ltd.

Mhando, P. na Balisidya, N. (1976). *Fasihi na Sanaa za Maonyesho*. Dar es Salaam. TPH.

Migodela, W. (2020). *Kuchunguza Mtindo katika Nyimbo za Tiba Asili: Mifano kutoka Nyimbo za Waganga wa Mkoa wa Ruvuma. Tasinifu za Uzamivu. (Haijachapishwa).* Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Dar es Salaam.

Mihale, K. P. (2011). *Ujumi katika Ushairi wa Mnyampala*. Tasinifu ya Shahada ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dododma .

Moore, H. T. (1976). *Realism and Naturalism*. London: Donald Pizzer

Mulokozi, M. M. (1996*). Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili, Kozi za Fasihi Vyuoni na Sekondari*. Dar es Salaam: Macony Printing.

Ponera, A. S. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*. Dar es Salaam: Kaarljamer Printing Technology.

Ponera, A. S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu*. Dodoma: Central TanganyikaPress

Renatus, S. (2018). *Ujumi wa Kiafrika Katika Tamthiliya ya Kiswahili. Mifano kutoka Kinjekitile na Mashetani. Tasinifu ya M.A (Haijachapishwa).* Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Russell, K. M. (2012) Introduction to African Art. Austin, TX: St. Andrew‘s Samwel, M., Amina, J.S., na Akech, J.K. (2013). *Ushairi wa Kiswahili Nadharia, Maendeleo, Mwongozo kwa Walimu wa Kiswahili na Diwani ya MEA*. Dar es Salaam: Mevel Publishers.

Sanga, A. N. (2012). *Ujumi katika Riwaya Pendwa ya Kiswahili: Mifano kutoka kwa Mohamed Said Abdulla na Arstablius Elvis Musiba*. Tasinifu ya Shahada ya Umahiri: Chuo Kikuu cha Dododma, Dodoma.

Sanga, A. N. (2018). *Mkengeuko wa Ujumi wa Kiafrika Katika Hadithi Fupi Andishi za Kiswahili Kipindi cha Utandawazi: Mifano Kutoka Magazeti ya Habari Leo, Nipashe na Mwananchi. Shahada ya Uzamivu (Hijachapishwa)*. Chuo Kikuu cha Dododma, Dododma

Sanga, A. N. (2021) Thamani ya Ujumi wa Kiafrika katika Hadithi Fupi Simulizi za Kiswahili: *Mulika Na. 40*(1): 80-96.

Senkoro, F. E. M. K. (1988). *Ushairi: Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press & Amin Education and Research Academy.

Senyamanza, C.R. (hnw) *Misingi ya Kazi za Kubuni, Nadharia, Mbinu na Mifano ya Kibunilizi*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.

Snow, C. P. (1968). *The Realists: Portraits of Eight Novelists*. London: Macmillan.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Wafula, R. M., na Njogu, K. (2007) Nadharia za Uhakiki wa Fasihi. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundtion.

Wamitila, K.W. (2003). *Fasihi Simulizi*. Nairobi: Muwa Publishers Limited.

Wamitila, K.W. (2004). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: English Press.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

Wamitila, K.W. (2010). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vude-Muwa Publishers Limited.

Yonazi, E. (2019). *Usanaa wa Lugha katika Ujenzi wa Dhima za Nyimbo za Harusi za Waasu. Tasinifu ya M.A Kiswahili (Haijachapishwa)*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam..

Zirimu, P. *(1973). Black Aesthetics*: Papers from a Colloquium Held at the University of Nairobi, June 1971, Nairobi.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.